# SERA HUDUMA ZA TEHAMA

# HOSPITALI YA JIJI ARUSHA

# YALIYOMO


**1.0 UTANGULIZI ........ 3**

**2.0 MALENGO ........ 3**

**3.0 MATUMIZI YA SERA ........ 3**

**4.0 SERA ........ 4**

**4.1 Huduma za Mifumo ........ 4**

**4.2 Matumizi ya Mtandao ........ 4**

**4.3 Ruhusa ya Matumizi ........ 4**

**4.4 Kutunza na kudhibiti Taswira ya Hospitali ........ 5**

**4.5 Kuratibu Usalama wa Taarifa (Periodic Data Back-Up) ........ 5**

**4.6 Kuzuia Matumizi yasiyofaa ........ 5**

**5.0 Maboresho / Mapendekezo ........ 5**

**5.1 Maboresho katika Masuala ya Mifumo ........ 6**

**5.2 Maboresho katika Masuala ya Mtandao ........ 6**

**5.3 Maboresho katika Masuala ya Vifaa na Miundombinu ya TEHAMA ........ 6**

**5.4 Maboresho katika Masuala ya Kutengeneza Taswira ya Hospitali (Hospital Public Reputation) ........ 7**

**Tovuti ya Hospitali:**

## 1.0 UTANGULIZI

Matumizi ya huduma za TEHAMA katika Taasisi ni mjumuiko wa matumizi ya Huduma za kiteknolojia zikiwemo matumizi ya huduma za mtandao, ulinzi, matumizi ya vifaa na masuala yote yanayohusu urekebishaji wa miundombinu ya kiteknolojia inayohusu huduma za TEHAMA katika Taasisi. Matumizi ya huduma za TEHAMA ina lengo la kuimarisha ubora wa utoaji wa huduma zinazopatikana katika hospitali ya Jiji Arusha zinazotolewa na watumishi / watoa huduma wanaopatikana. Pia, kuhakikisha matumizi ya huduma za mtandao ndani ya Hospitali ya Jiji Arusha inafanyika kwa ufanisi mkubwa miongoni mwa watoa huduma kwa wagonjwa wanaofika kwa ajili ya kupata matibabu. Hivyo kuepuka uharibifu wa miundombinu ya kiusalama iliyoweka katika Hospitali ya Jiji Arusha

Kwa mantiki hii, huduma za TEHAMA zitaruhusiwa kwa watumishi wa Hospitali pekee ili kuimarisha utoaji wa huduma kulingana na taaluma zao katika sekta ya Afya.

## 2.0 MALENGO

Malengo ya sera Huduma za TEHAMA ni kutoa ufafanuzi, kuhakikisha na kusimamia matumizi yote ya huduma za TEHAMA zinazopatikana katika ***Hospitali ya Jiji Arusha*** kwa watumishi wote.

## 3.0 MATUMIZI YA SERA

Sera imeandaliwa kwa lengo la kutumika ndani ya Hospitali ya Jiji Arusha kwa watumishi wake wote. Ikiwa neno “Watumishi” likiwa na maana pana ambayo ni wale watumishi wa Muda wote(full-time) , watumishi wa muda mfupi(part-time), watumishi wa mkataba (contract-based) na wadau mbalimbali katika kuhakikisha utoaji wa huduma katika hospitali ya Jiji Arusha unakuwa wa kiwango cha hali nzuri kwa kuzingatia matumizi ya huduma za mtandao zinazoendana na majukumu yao ya kazi za kila siku.

Pia, watumishi wanatakiwa wawe na uelewa na sera huduma za TEHAMA ikiwa kama muongozo wa matumizi ya huduma za TEHAMA katika hospitali ya Jiji Arusha.

## 4.0 SERA

### 4.1 Huduma za Mifumo

Sera ina lengo la kuhakikisha mifumo inayotumika / itakayotumika katika utoaji wa huduma za Afya katika hospitali ya Jiji Arusha inafanya kazi katika ufanisi wa hali ya juu. Pia, kuhakikisha utoaji wa msaada pale utakapokuwa unahitajika katika kutengeneza, kurekebisha au kutoa ubunifu zaidi unaohusu mifumo ya utoaji wa huduma ndani ya hospitali ziweze kupatikana kwa urahisi na ufanisi wa hali ya juu. Hivyo, kuhakikisha taarifa zilizokusudiwa kukusanywa kutokana na matumizi ya mifumo zinakuwa katika kiwango cha ulinzi wa hali ya juu miongoni mwa watumishi ambao wanatumia mifumo hiyo

Pia, kukumbusha masuala ya kiusalama wa mifumo hasa kwa watumishi ambao ndio walengwa wakubwa wa matumizi ya mifumo katika utoaji wa huduma ndani ya hospitali ya Jiji Arusha bila kuruhusu upotevu wa taarifa yoyote inayohusu taaluma zao katika kada ya Afya.

### 4.2 Matumizi ya Mtandao

Sera ina lengo la kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya mtandao, pia watumishi ndani ya hospitali ya Jiji Arusha wawe na uwezo wa kutumia huduma za mtandao ikiwa ni msaada katika utekelezaji wa majukumu yao. Hivyo, watumishi waweze kutumia huduma ya mtandao kwa ajili ya matumizi ya kiofisi tu kaitka utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku kwa ufanisi wa hali ya juu. Hivyo, kuwe na udhibiti wa matumizi ya huduma ya mtandao.

Matumizi ya Mtandao yakiwemo yafuatayo;

- Matumizi ya WiFi (Non-Cabled Internet)
- Uboreshwaji na Matumizi ya Simu (Telephones Configurations)

### 4.3 Ruhusa ya Matumizi

Sera ina lengo la kuruhusu matumizi ya huduma za mtandao kwa huduma za kiofisi kwa lengo la kuimarisha utoaji huduma katika hospitali ya Jiji Arusha. Hivyo, watumishi watakuwa na uwezo wa kutumia miundombinu ya mtandao kwa ajili ya kukamilisha majukumu yao ya kila siku wawapo ndani ya hospitali ya Jiji Arusha. Pia, pindi watakapokuwa wanahitaji msaada waweze kupatiwa kulingana na vitengo vyao kwa kuzingatia mambo muhimu yafuatayo;

- Kuhitaji na kupata taarifa
- Kuhitaji na kupata msaada wa kurekebisha huduma katika kuimarisha utoaji huduma (Software upgrading & Hardware Maintenance)

## 4.4 Kutunza na kudhibiti Taswira ya Hospitali

Sera in lengo la kutunza na kudhibiti taswira ya hospitali ndani na nje. Kwa kuzingatia masuala ya matangazo (Vipeperushi, tovuti, mabango, videos) kwa kuzingatia matumizi ya huduma za TEHAMA vinavyohusu huduma zinazopatikana katika hospitali ili watu wawe na uelewa.

## 4.5 Kuratibu Usalama wa Taarifa (Periodic Data Back-Up)

Pia Sera ina lengo la kuweka utaratibu wa kuratibu usalama wa taarifa mara kwa mara ili kuzuia upotevu wa taarifa muhimu pindi zinapohitajika. Utaratibu wa kufanya uratibu wa usalama wa taarifa za Hospitali ya Jiji Arusha kwa kuzingatia kipindi Fulani cha muda (Time Interval) zikijumuisha katika vipengele vifuatavyo;

- Mfumo wa GoT-HoMIS ( Usalama wa Taarifa)
- Uhakiki wa ufanyaji kazi Mfumo wa GoT-HoMIS Masaa 24 ( 24Hrs)
- Mfumo wa Kusign kwa Alama ya Kidole (Biometric System)
- Staff Files/ Folder Access
- Periodic CCTV Camera Data Back-up (24 Hrs running)
- Internet Access Data Back-Up

## 4.6 Kuzuia Matumizi yasiyofaa

Sera ina lengo la kuzuia matumizi yasiyofaa ikizingatiwa yale yenye uhusiano na matumizi ya huduma za TEHAMA ndani ya Hospitali ya Jiji Arusha. Baadhi ya Matumizi hayo ni yafuatayo;

- Kutumia miundombinu na vifaa vya TEHAMA kinyume na dhumuni la huduma zinazotolewa ndani ya Hospitali ya Jiji Arusha
- Kudukua au kuzuia kutumika kwa maudhui ya hospitali kinyume na sheria
- Kuzuia ufanyikaji wa uhalifu wa kimtandao katika hospitali ya Jiji Arusha
- Kuzuia kupakua/ downloading au kusambaza taarifa zinazoweza kuharibu taswira ya Hospitali ya Jiji Arusha mitandaoni (Virus)

## 5.0 Maboresho / Mapendekezo

Sera ina lengo la kuelezea na kupendekeza ni maboresho yapi yangefanyika katika huduma za TEHAMA ili kuboresha huduma zinazotolewa ndani ya hospitali ya Jiji Arusha. Miongoni mwa maboresho hayo yamegawanyika katika vipengele vifuatavyo;

- Maboresho katika Masuala ya Mifumo
- Maboresho katika Masuala ya Mtandao
- Maboresho katika Masuala ya Kurekebisha vifaa na Miundombinu ya TEHAMA

## 5.1 Maboresho katika Masuala ya Mifumo

Sera ina lengo la kufafanua ni maboresho gani yanafaa kufanyika katika masuala ya Mifumo TEHAMA ili kuboresha utoaji wa huduma katika Hospitali ya Jiji Arusha. Baadhi ya maboresho pendekezwa katika masuala ya Mifumo ni kama ifuatavyo;

i. Uundaji, ubunifu na utengenezwaji wa Tovuti (Website) ya Hospitali ya Jiji Arusha. Ni mfumo ambao utawezesha kutoa taswira ya Hospitali ya Jiji Arusha ikiwemo kuelezea huduma zinazopatikana ikijumuisha maelezo yanayoweza kumpa uelewa mgeni / mpokea huduma kupitia mtandao (Internet) kwa urahisi
ii. Uundaji, ubunifu na utengenezwaji wa Mfumo wa Kanzidata / Database ya Wakuu wa Idara na watumishi wengine. Mfumo utakaowawesha kuhifadhi taarifa zao za vikao, mikutano na taarifa nyingine watakazozihitaji kwa matumizi ya baadae pamoja na kupokea taarifa mbalimbali kutoka kwa Uongozi kwa urahisi
iii. Uundaji, ubunifu na utengenezaji wa Mfumo wa kukusanya maoni ya kuboresha kutoka kwa watumishi wa hospitali ya Jiji Arusha
iv. Kuwa tayari kutoa mawazo ya kuboresha zaidi ufanyaji kazi wa mfumo wa GoT-HoMIS unaotumiwa na watoa huduma

## 5.2 Maboresho katika Masuala ya Mtandao

Pia Sera ina lengo la kufafanua ni maboresho gani yanafaa kufanyika katika masuala ya Mtandao ikiwa na lengo la kuboresha utoaji wa huduma katika hospitali ya Jiji Arusha. Baadhi ya maboresho hayo yakijumuisha yafuatayo;

i. Ufanyikaji wa matengenezo ya Matumizi ya Simu za Mezani ( Telephone Configuration)
ii. Uundaji wa matumizi ya Mtandao ( Wireless Connectivity) kwa watumishi ndani ya hospitali ya Jiji Arusha

## 5.3 Maboresho katika Masuala ya Vifaa na Miundombinu ya TEHAMA

Sera ina lengo la kufafanua ni maboresho gani yanafaa kufanyika katika masuala ya Vifaa na Miundombinu ya TEHAMA ikiwa na lengo la kuboresha utoaji wa huduma katika hospitali ya Jiji Arusha. Baadhi ya maboresho hayo ni kama ifuatavyo;

i. Kutenganisha miundombinu ya CCTV Camera na Matumizi ya Mtandao kwa shughuli za kila siku kwa watumishi. WiFi Router kwa ajili ya CCTV Camera na WiFi Router kwa matumizi ya kila siku kwa watumishi
ii. Uboreshwaji wa baadhi ya vifaa vyenye uwezo mzuri wa ufanyaji kazi katika mazingira ya Server kama vile UPS ( Uninterruptible Power Supply ) kuhakikisha server inafanya kazi masaa 24 ( Muda wote)

## 5.4 Maboresho katika Masuala ya Kutengeneza Taswira ya Hospitali (Hospital Public Reputation)

Sera ina lengo la kufafanua ni maboresho gani yanafaa kufanyika yakiwa na lengo la kujenga na kuimarisha taswira ya Hospitali ya Jiji Arusha. Miongoni mwa maboresho yanayofaa kufanyika yakijumuisha yafuatayo;

i. Kutengeneza akaunti za mitandao ya kijamii za Hospitali ya Jiji Arusha zikiwemo Akaunti za Instagram na Youtube zikiwa na lengo la kuhabarisha jamii kuhusu huduma zinazopatikana na matukio yaliyotokea katika hospitali ya Jiji Arusha. Ikiwa ni sehemu ya kuimarisha Mahusiano na taswira kwa watu wa nje ya hospitali ( Public relations)
ii. Kuunda na kutengeneza Vipeperushi na matangazo yakiwa na lengo la kuhabarisha watu wa nje ya hospitali kuhusu huduma zinazopatikana zikiwemo huduma zinazopatikana katika kila kitengo ndani ya hospitali ya Jiji Arusha
iii. Pia, kuunda na kutengeneza miundombinu mbalimbali katika kuhakikisha taswira ya hospitali inaimarishwa na kuongeza ufahamu kwa watu nje ya hospitali ya Jiji Arushajuu ya huduma zinazopatikana.